
NYARAKA 1

COMIC BIBLE
SOCIETY

Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2023

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


WARUMI
ROMA ILIKUWA JIJI KUU NA MJI MUHIMU KWA YOTE KWA UFALME WA ROMA.
WENGINE WALIOBADILI SIKU YA PENTEKOSTE [1] YAWEZEKANA WALIANZISHA KANISA LA ROMA.
[1] MATENDO 2:10
PAULO ALIKUWA HAJATEMBELEA ROMA NA ALIKUSUDIA KUFANYA HIVYO AKIENDA UHISPANIA.
HAKUANDIKA BARUA HII KUREKEBISHA THEOLOGIA ILIYOKUWA NA MAKOSA KWA SABABU KANISA ILIKUWA NA MTAZAMO SAHIHI WA BIBLIA, ILA KANISA HII, KAMA KANISA ZOTE, ILIHITAJI MAFUNDISHO MAZURI.
NIA YAKE ILIKUWA KUFUNZA INJILI YA NEEMA KWA WAUMINI WA ROMA AMBAO HAWAKUWA WAMEPATA MAFUNDISHO KUTOKA KWA MITUME.
KATIKA BARUA HII AELEZEA AMBAVYO MUDA WA KRISTO ULIMWENGUNI UNAUNGANA NA KAZI YA MUNGU KATIKA HISTORIA YA WAYAHUDI NA KWA SIKU ZA USONI KWA BINAADAMU.
ILIYOTOLEWA IMLA KWA MWANDISHI ALIYEITWA TERTIO, WARUMI NI KITABU KIREFU ZAIDI KATIKA BARUA ZA MTUME KIKIWA NA MANENO 7,000.



UONGOZI WA KIROHO
NAMSHUKURU MUNGU KUPITIA YESU KRISTO KWA RIPOTI HII NZURI, NA KWA KILA MMOJA WENU.
KILA NIENDAKO NASIKIA KUHUSU IMANI YENU - INAANZA KUJULIKANA KWOTE ULIMWENGUNI.
NAENDELEA KUOMBEA FURSA YA KUJA KUWAONA.
NATAKA KUGAWA IMANI YANGU NANYI NA KUTIWA MOYO NA YENU.
KWA MAANA SIIONEI HAYA INJILI YA HABARI NJEMA JUU YA KRISTO - NI NJIA YA MUNGU YA WOKOVU.
UJUMBE HUU ULIHUBIRIWA KWANZA KWA WAYAHUDI, LAKINI SASA KILA MMOJA AALIKWA KUJA KWA MUNGU KWWA NJIA HII HII.
HASIRA YA MUNGU DHIDI YA DHAMBI
"LAKINI MUNGU AONYESHA HASIRA YAKE KUTOKA MBINGUNI DHIDI YA WATU WOTE WENYE DHAMBI WANAOSUKUMA KANDO UKWELI."
"AMEUWEKA UKWELI WAKE KWENYE MIOYO YENU, ILI WASIWE NA SABABU WASIMAMAPO MBELE Y MUNGU SIKU YA HUKUMU."
"LAKINI HAWAWEZI KUKUBALI."
"BADALA YA KUMUABUDU MUNGU MTUKUFU, WALICHUKUA MBAO NA MAWE NA KUJITENGENEZEA MIUNGU."


"KWA HIYO WAKAANZA KUFANYA VITU VIBAYA NA VYA DHAMBI."
"BADALA YA KUAMINI WALICHOKIJUA KILIKUWA UKWELI JUU YA MUNGU; WALICHAGUA KUSUDI KUAMINI UONGO."
"KWA HIYO MUNGU AKAWAACHA WAFANYE VITU VIOVU - HATA WAKE WAO WALIGEUKA DHIDI YA MPANGO ASILI WA MUNGU."
"NA WAUME WAO WALIFANYA VITU VYA AIBU NA WAUME WENGINE."
"WALIKATAA KUWA NA MUNGU KATIKA FAHAMU ZAO, ALIWAACHA WAFANYE KILA KIOVU WALICHOWEZA KUKIFIKIRIA."
"WAMEJAWA NA KILA AINA YA DHAMBI - TAMAA, CHUKI, WIVU, UUAJI, FITINA, HADAA, UCHUNGU NA KUSENGENYA."
"WENYE KUMCHUKIA MUNGU, WAJEURI, WENYE MAJIVUNO, WENYE KUTUNGA MABAYA, WASIOWATII WAZAZI WAO."
"WALIFAHAMU SANA HUKUMU YA HAKI YA MUNGU KWA HAYA YOTE LAKINI WALIYAFANYA VIVYO HIVYO."
WARUMI 1:24-32


KANUNI ZA HUKUMU YA MUNGU
"WAWEZA KUWA WASEMA, 'WATU WAOVU KWELI!' LAKINI NGOJA KIDOGO! WEWE PIA NI MUOVU."
"USEMAPO NI WAOVU NA WANAFAA KUADHIBIWA, WAJIZUNGUMZIA MWENYEWE, KWA KUWA WAVIFANYA VITU HIVI HIVI."
"MUNGU, KWA HAKI, ATAMUADHIBU YEYOTE AFANYAYE VITU KAMA HIVI."
"HAUONI MUNGU ALIVYO MVUMILIVU?"
"AMEKAA WAKATI HUU WOTE BILA KUKUADHIBU - UKARIMU WAKE UNAFAA UKUONGOZE KWA TOBA."
UKWELI WA DHAMBI
"BASI TENA, JE SISI WAYAHUDI NI ZAIDI YA WENGINE? LA, HASHA, KWANI TUSHAONYESHA KUWA WATU WOTE WAKO SAWA KAMA WENYE DHAMBI, WAWE WAYAHUDI AU WAYUNANI."
"KILA MMOJA AMEASI; WOTE WAMEENDA MRAMA. HAKUNA MMOJA POPOTE AMEENDELEA KUFANYA KILICHO SAWA; HATA MMOJA."
WARUMI 2:1-3:20


KUHESABIWA HAKI NA IMANI PEKE YAKE
"LAKINI SASA MUNGU AMETUONYESHA HATUFIKI MBINGUNI KWA 'KUWA WAZURI IPASWAVYO' NA KUJARIBU KUFUATA SHERIA ZAKE, ILA KWA NJIA MPYA."
"SASA MUNGU ASEMA 'HATUNA HATIA'-TUKIMUAMINI YESU KRISTO KUONDOA DHAMBI ZETU."
"NA SOTE TWAWEZA KUOKOLEWA KWA NJIA HII, KWA KUJA KWA KRISTO, HAIJALISHI SISI NI NANI AMA TULIVYOKUWA - KWA MAANA WOTE WAMETENDA DHAMBI NA KUPUNGUKIWA NA UTUKUFU WA MUNGU."
DHAMANA YA WOKOVU
"HIVI SASA KWA KUWA TUMEWEKWA SAWA KWA MACHO YA MUNGU KWA IMANI KATIKA AHADI ZAKE, TWAWEZA KUWA NA AMANI NAYE KWA SABABU YA KILE ALICHOTUFANYIA YESU KRISTO."
"KWA MAANA HAPO TULIPOKUWA HATUNA NGUVU, WAKATI ULIPOTIMIA KRISTO ALIKUF KWA AJILI YETU."
"SASA TUNAFURAHIA NDANI YA UHUSIANO WETU MPYA-YESU KRISTO AMEKUFA KWA AJILI YA DHAMBI ZETU NA KUTUFANYA MARAFIKI WA MUNGU."


UHAMISHO WA DHAMBI YA ADAMU
"ADAMU ALIPOTENDA DHAMBI, DHAMBI ILIINGILIA WANADAMU."
"DHAMBI YAKE ILIENEA ULIMWENGUNI KOTE, KWANI WOTE WALITENDA DHAMBI."
"ADAMU, ALIWALETEA WENGI KIFO KUPITIA DHAMBI YAKE."
"ILA MTU MMOJA, YESU KRISTO, ALILETA MSAMAHA KWA WENGI KUPITIA REHEMA YA MUNGU."
UTAKASO
"TUDUMU KATIKA DHAMBI ILI MUNGU ATUONYESHE MSAMAHA KWA WINGI?"
"HASHA! KWA KUWA NGUVU ZA DHAMBI JUU YETU ZILIVUNJWA TULIPOKUWA WAKRISTO NA KUBATIZWA ILI KUWA SEHEMU YA YESU KRISTO."
"NAFSI ZENU ZINAZOPENDA DHAMBI ZILIZIKWA NAYE KWA UBATIZO HADI KIFO NA WAKATI MUNGU BABA ALIMREGESHA KUWA HAI TENA - MLIPEWA MAISHA MAPYA."
"VILE AMBAVYO MLIKUWA WATUMWA KWA KILA AINA YA DHAMBI, BASI SASA LAZIMA MUWE WATUMWA KWA KILA KILICHO SAWA NA KITAKATIFU."
"KWA MAANA MSHAHARA WA DHAMBI NI MAUTI, BALI KARAMA YA MUNGU NI UZIMA WA MILELE KATIKA YESU KRISTO BWANA WETU."
WARUMI 5:12 - 6:20


"KWANI HUELEWI KUWA MTU ANAPOKUFA TORATI HAIMTAWALI TENA?"
"WAKATI MWANAMKE AMEOLEWA, AMEFUNGWA KWA MUMEWE WAKATI ANAPOKUWA YU HAI - BALI AKIFA, HAJAFUNGWA KWAKE TENA."
"'MUMEO' ALIKUWA TORATI LAKINI 'ULIKUFA' NA KRISTO MSALABANI NA 'HAUJAOLEWA NA TORATI' TENA."
"MULIFUFUKA KRISTO ALIPOFUFUKA, SASA MU WATU WAPYA."
"TORATI NI NJEMA - SHIDA SIO TORATI ILA MIMI - KWANI NIMEUZWA KWA DHAMBI KAMA MTUMWA."
"NATAMANI SANA KUTENDA MEMA - ILA NAFANYA NISICHOTAKA KUKIFANYA - NINAVYOVICHUKIA."
"MAISHA YANGU MAPYA YANIAMBIA NITENDE MEMA, LAKINI TABIA YA ZAMANI ILIYOKO BADO NDANI YANGU YAPENDA KUTENDA DHAMBI."
"SASA BASI HAKUNA HUKUMU YA ADHABU KWA SABABAU YESU KRISTO AMENIWEKA HURU."
"KWANI NIMESHAJUA KWA HAKIKA HAKUNA KINACHOWEZA KUTUTENGANISHA NA UPENDO WAKE."
"WALA MAUTI, WALA UZIMA, WALA MALAIKA, WALA MAPEPO, WALA UWOGA, WALA WASIWASI, WALA YALIYO JUU, WALA YALIYO CHINI VITATUTENGA NA UPENDO WA MUNGU ALIOTUONYESHA KATIKA BWANA WETU YESU KRISTO."


UCHAGUZI WA ENZI
"EH WATU WA ISRAELI - MDA GANI MPAKA MJE KWA KRISTO!"
"NIKO TAYARI KULAANIWA MILELE KAMA HIYO ITAWAOKOA."
"MUNGU AMEWAPA MENGI SANA - BALI HAMTAMSIKIZA."
"ALIWACHAGUA KAMA WATU WAKE NA KUWAONGOZA NA WINGU LA UTUKUFU."
"ALIWAPA AMRI ZAKE NA KRISTO MWENYEWE ALIKUWA MMOJA WENU - MYAHUDI UBINADAMU WAKE UNAPOHUSIKA."
MPANGO WA MUNGU KWA ISRAELI
"NABII ISAYA ALILIA..."
INGAWA NAMABARI YA WAISRAELI NI KAMA MCHANGA UFUONI MWA BAHARI - WALIOBAKI PEKE YAO NDIO WATAOKOLEWA.
"MUNGU AMEWAPA FURSA WAYUNANI KUACHILIWA HURU NA IMANI."
"WAYAHUDI HAWAKUFAULU KWA SABABU WALIKUWA WANAJARIBU KUOKOLEWA KWA KUFUATA SHERIA BADALA YA KUTEGEMEA IMANI."
"MUNGU HAJAWAKATAA WATU WAKE ALIOWACHAGUA KUTOKA MWANZO KABISA."
"KUSUDIO LAKE LILIKUWA KUFANYA UOKOVU UWEZE KUPATIKANA KWA WAYUNANI, KISHA WAYAHUDI WANGEANZA KUJITAKIA UOKOVU WA MUNGU."


KARAMA ZA KIROHO
"NAWASIHI, ITOENI MILI YENU IWE DHABIHU ILIO HAI - TAKATIFU NA YA KUMPENDEZA MUNGU."
"JIFIKIRIENI KWA MAWAZO YA KIASI, KULINGANA NA IMANI ALIYOWAPATIA MUNGU."
"KAMA VILE MWILI WETU UNA VIUNGI VINGI BASI HIVYO SOTE TU VIUNGO VYA MWILI WA KRISTO NA KAZI TOFAUTI KUUFANYA MWILI UKAMILIKE."
"IKIWA MUNGU AMEKUPA UWEZO WA UNABII - BASI NABII KWA KADIRI YA IMANI ANAYOKUPA."
"KAMA WEWE NI MWALIMU - FANYA KAZI NJEMA KUFUNZA."
"IKIWA HUDUMA - WAHUDUMIE WENGINE VYEMA."
"KAMA WEWE NI MHUBIRI - HUBIRI MAHUBIRI YA NGUVU NA YANAYOSAIDIA."
"KAMA MUNGU AMEKUPA UTAJIRI - KUWA MKARIMU KWA WENGINE."
"KAMA MUNGU AMEKUPA MAMLAKA - TILIA MAKINI JUKUMU HILO."
"KAMA NIKUONYE-SHA REHEMA - FANYA KWA FURAHA."
WARUMI 12:1-8



UCHA MUNGU KWA VITENDO
"USIJIDAI TU KUWAPENDA WENZAKO: WAPENDE KIKWELI."
"USIWAHI KUWA MVIVU KWENYE KAZI YAKO BALI MTUMIKIE BWANA KWA SHAUKU."
"KUWENI WENYE SUBIRA KWA DHILI NA MUSALI WAKATI WOTE."
"WAKATI WANA WA MUNGU WAKO KATIKA UHITAJI WASAIDIENI."
"MTU AKIKUTESA KWA KUWA U MKRISTO USIMLAANI; OMBA KUWA MUNGU ATAMBARIKI."
"MSIJIPENEKEZE KWA WATU WA MAANA BALI FURAHIKIA KUJUMUIKA NA WATU WA KAWAIDA."
"MSILIPE MABAYA KWA MABAY - ACHENI WATU WAONE UAMINIFU KWA SHUGHULI ZENU."
"MSIGOMBANE BALI MUWE NA AMANI NA KILA MTU KADRI INAVYOWEZEKANA."
HA HA
"LAKINI, ADUI YAKO AKIWA NA NJAA MLISHE."
"AKIWA NA KIU MPE CHA KUNYWA - USHINDE UBAYA KWA KUTENDA WEMA."
WARUMI 12:9-12


JUKUMU KWA SERIKALI YA KIBINADAMU
"TII SERIKALI, KWANI MUNGU NDIYE ALIYEIWEKA HAPO."
"WANAOKATAA KUTII SHERIA WANAKATAA KUMTII MUNGU, NA ADHABU ITAFUATIA."
"LIPA USHURU WAKO ILI WAFANYAKAZI WA SERIKALI WAWEZE KUENDELEA KUFANYA KAZI YA MUNGU KWA KUKUTUMIKIA WEWE."
"MLIPE KILA MMOJA ANACHOSTAHILI - PEANA HESHIMA KWA WALE WANAOSTAHILI."
"LIPA MADENI YAKO YOTE ISIPOKUWA DENI LA UPENDO KWA WENGINE-USIWAHI KUMALIZA KULIPA HILO!"
"AMRI ZOTE KUMI ZIMEFINIKWA KATIKA HII - MPENDE JIRANI YAKO UNAVYOJIPENDA MWENYEWE."
"SABABU NYENGINE YA KUISHI MAISHA SAWA NI HII - KURUDI KWA BWANA KUMEKARIBIA SASA ZAIDI YA PALE TULIPOAMINI KWA MARA YA KWANZA."
"USITUMIE WAKATI WAKO KWA SHEREHE ZA ANASA NA KULEWA AU KWA KUZINI NA TAMAA AU KUPIGANA AU WIVU."
"LAKINI MUULIZE BWANA YESU KRISTO AKUSAIDIE KUISHI UNAVYOPASWA."



KANUNI ZA UHURU WA KIKRISTO
"MKARIBISHE NDUGU YEYOTE ANAYETAKA KUJIUNGA NANYI, HATA KAMA IMANI YAKE I DHAIFU."
"USIMKASHIFU KWA KUWA NA MAWAZO TOFAUTI KUHUSU KILICHO SAWA NA KILICHO MAKOSA."
"HUNA HAKI YA KUMKASHIFU NDUGU YAKO AU KUMDHARAU."
"KUMBUKA KILA MMOJA WETU ATASIMAMA MBELE YA KITI CHA HUKUMU NA KUTOA RIPOTI YAKE MWENYEWE KWA MUNGU."
"JARIBU KUISHI KWA NJIA AMBAYO HAUTAWAHI KUMKWAZA NDUGU YAKO KWA KUMUACHA AKUONE UKIFANYA JAMBO ANALOLIDHANIA NI MAKOSA."
"HATA KAMA TUNAFIKIRIA HAKUNA TOFAUTI YOYOTE KWA BWANA, HATUWEZI KUJIFURAHISHA WENYEWE TU - LAZIMA TUZINGATIE SHAUKU NA HOFU ZA WENGINE."
"NA MUNGU ANAYETOA SABURI, UTHABITI NA KUTIA MOYO AWASAIDIE MUISHI KWA MAELEWANO - NA MTAZAMO WA KRISTO KWA KILA MMOJA."
"NAMKABIDHI FIBI, DADA YETU ANAYELETA BARUA HII."
"WASALIMIE WOTE KANISANI."
"KWA MUNGU MWENYE HEKIMA PEKE YAKE UWE UTUKUFU KUPITIA KWA YESU KRISTO MILELE"



I, II WAKORINTHO
B.K. 55. KANISA LA KORINTHO LILIKUWA NA SHIDA - SHIDA NYINGI.
KANISA HAPO LILIANZISHWA NA MTUME PAULO KWENYE SAFARI YAKE YA PILI YA KIMISHONARI.
BAADA YA KUONDOKA KORINTHO ALISIKIA KUHUSU KUZINI KANISANI NA AKAANDIKA INAYOITWA "BARUA KALI." (I WAK.5:9)
KISHA, KUYAJIBU MASWALI MENGINE KANISA ILIKUWA NAYO, AKAANDIKA BARUA HII. (I WAKORINTHO)
MJI ULIKUWA UMEHARIBIKA KIMAADILI, HATA KWA KIWANGO CHA KIDUNIA, MPAKA JINA KORINTHO LIKALINGANISHWA NA UFISADI NA KUHARIBIKA KWA MAADILI.
SHIDA KUBWA KABISA KWENYE KANISA ILIKUWA ULIMWENGU - KUTOTAKA KUJITENGA NA TAMADUNI ZILIZOWAZINGIRA.
KATIKAKATI YA HAYA, PAULO ALIPANDA KANISA NA KUWAFUNZA KUISHI KAMA WAKRISTO.
"TAZAMA NDUGU, WACHACHE WENU WANAOMFUATA KRISTO WANA MAJINA MAKUBWA AU MAMLAKA AU UTAJIRI."
"BADALA YAKE MUNGU ALIWACHAGUA WALE ALIOWACHUKULIA WANYONGE ILI HAKUNA ATAKAYEJIVUNA MBELE YAKE."


NILIPOKUJA KWENU SIKUTUMIA MANENO MATAMU NA DHANA KUU ILA NILIZUNGUMZIA YESU KRISTO NA KIFO CHAKE MSALABANI PEKE YAKE - ILI IMANI YENU ITUE KWA MUNGU SIO KWA MANENO YA MWANADAMU.
KAMA WATU WAKUU WA ULIMWENGU WANGEELEWA, HAWANGEMSULUBISHA BWANA WA UTUKUFU.
MAANDIKO YANAYOSEMA KUWA HAKUNA MTU WA KAWAIDA AMEWAHI KUONA, AU KUSIKIA, AU HATA KUWAZA MAMBO YA AJABU MUNGU AMEWATAYARISHIA WALE WAMPENDAO BWANA.
MNAPOKUWA NA WIVU NA KUGOMBANA, MNAJIFANYA KAMA WATU AMBAO SIO WA BWANA KABISA.
"MSIWE NA WEPESI WA KUJIAMULIA KAMA MTU NI MTUMISHI MZURI AU LA."
"BWANA ATAKAPORUDI ATADHIHIRISHA KILICHO KWELI NDANI YA MIOYO YETU."
"SIANDIKI KUWAAIBISHA ILA KUWASHAURI KAMA WATOTO WAPENDWA."
"FUATA MFANO WANGU NA FANYA NIFANYAVYO."


"KUNA UASHERATI KATI YENU AMBAO HATA WATU WA DUNIA HAWAFANYI - MWANAMUME ANAISHI NA MKE WA BABA YAKE."
"LAZIMA MUMTOE MWANAMUME HUYU KWA USHIRIKA WENU - NA MATUMAINI KUWA ATAOKOLEWA."
"NILIPOWAANDIKIA MBELENI NA KUSEMA MSICHANGANYIKANE NA WATU WAOVU - NILIKUWA SIZUNGUMZII WASIOAMINI."
"NILIMAANISHA MSIFUATANE NA YEYOTE ANAYEDAI KUWA MKRISTO LAKINI ANAZINI, ANA TAMAA, TAPELI, MLEVI AU ANABUUDU MIUNGU."
"HATUKUMU WATU WA NJE - ILA TU WALE WALIO WASHIRIKI WA KANISA WANAOTENDA DHAMBI HIVI."
"NA KWA NINI MNASHTAKIANA - KWANI HAMJUI TUTAWAHUKUMU MALAIKA?"
“KUWA NA MASHTAKA KAMA HAYA NI KUSHINDWA KAMA WAKRISTO."
"WANAOABUDU MIUNGU, WAZINIFU, MASHOGA, WEZI, WENYE TAMAA, WALEVI, WACHONGEZI AU WAHUNI HAWATAKUWA NA KIPANDE KATIKA UFALME WAKE."
"WAKATI MMOJA MLIKUWA HIVYO ILA SASA DHAMBI ZENU ZIMEOSHWA NA NYINYI NI WA MUNGU."
"MILI YETU HAIKUTENGENEZEWA DHAMBI YA NGONO."
"TOROKA DHAMBI YA NGONO KWA SABABU NI DHIDI YA MWILI WAKO."



"SWALI LENU KUHUSU NDOA - NI VYEMA KUOLEWA, KWA SABABU BILA HIVYO MWAWEZA KURUDI KWA DHAMBI."
"KAMA MKRISTO ANA MKE ASIYE MKRISTO LAKINI ANATAKA KUKAA NAYE, HAFAI AMUACHE AU KUMTALIKI."
"NA VIVYO HIVYO MWANAMKE MKRISTO AMBAYE ANA MUME ASIYE MKRISTO."
"JAMII IKITENGANA, WATOTO WANAWEZA WASIWAHI KUMJUA BWANA - AMBAPO JAMII ILIYO PAMOJA INAWEZA KUISHIA KWA UOKOVU WA WATOTO."
"MKE NI SEHEMU YA MUME KWA MDA ALIO HAI, BWANAKE AKIFA BAI AWEZA KUOLEWA TENA ILA TU AOELEWE NA MKRISTO."
"KWENYE SWALI LENU KUHUSU CHAKULA KINACHOTOLEWA KAFARA KWA MIUNGU - TUNAJUA KUWA MIUNGU SIO MUNGU."
"KUNA MUNGU MMOJA TU, BABA, ALIYEUMBA VITU VYOTE NA BWANA YESU KRISTO, ALIYEUMBA VYOTE NA KUTUPA UHAI."
"WAKRISTO WENGINE WANAIFIKIRIA MIUNGU KAMA I HAI KWA HIYO KULA VYAKULA HIVYO VINATATIZA NAFSI ZAO."
"TAHADHARI MSITUMIE HURU WENU WA KULA - ISIJE MKASABABISHA NDUGU YENU AMBAYE NI MNYONGE KUWALIKO KUFANYA DHAMBI."


"ROHO MTAKATIFU ANAMPA KILA MMOJA KARAMA TOFAUTI."
"WENGINE HEKIMA, WENGINE WANAWEZA KUFUNZA, WENGINE WAWEZA KUPONYA, WENGINE WANA IMANI MAALUM, WENGINE MIUJIZA, WENGINE UWEZO WA KUHUBIRI NA WENGINE UWEZO WA KUZUNGUMZA NDIMI AMBAZO HAKUFUJIFUNZA."
SASA - WACHA NIWAONYESHE NJIA BORA.
KAMA NAWEZA KUZUNGUMZA LUGHA ZENGINE ILA SIWAPENDI WENGINE - NAPIGA KELELE TU.
KAMA NAUJUA WAKATI UJAO ILA SIWAPENDI WENGINE, ITANIFAA NINI?
"HATA NINGALIKUWA NA IMANI YA KUISONGEZA MILIMA WALA SINA UPENDO HAIMAANISHI CHOCHOTE."
"NIKITOA KILA NINACHO KWA MASIKINI NA KUCHOMWA NINGALI HAI KWA KUHUBIRI WALA SIWAPENDI WENGINE, HAITAKUWA NA THAMANI YOYOTE KAMWE."
"UPENDO HUVUMILIA NA HUFADHILI, HAUNA WIVU, HAUHUSUDU, HAUTAKABARI WALA KUJIVUNA, HAUNA KIBURI WALA UBINAFSI WALA JEURI."
"UPENDO HAUTAFUTI MAMBO YAKE. HAUKASIRISHWI WALA KUUDHIKA."
"HAUHESABU MABAYA NA HAUTAJALI IWAPO WENGINE WATAIKOSEA."
NILIPOKUWA MTOTO MCHANGA NILISEMA KAMA MTOTO MCHANGA, NILIFAHAMU KAMA MTOTO MCHANGA LAKINI NIKAWA MTU MZIMA NA KUYAWEKA MAMBO YA KITOTO NYUMA YANGU."
"KUNA VITU VITATU VITAKAVYODUMU-IMANI, TUMAINI, NA UPENDO-NA KUU KWA HAYA NI UPENDO."



"FUATENI UPENDO NA KUTAKA SANA KARAMA ZA ROHONI AMBAZO ROHO MTAKATIFU ANATOA, HASA KARAMA YA UNABII, UWEZO WA KUHUBIRI UJUMBE WA MUNGU."
"KAMA MNAAMINI KRISTO ALIFUFUKA KUTOKA MAUTI, KWA NINI WENGINE WENU WASEMA KUWA WALIOKUFA HAWATAWAHI KUWA HAI TENA?"
"KWANI KAMA HAKUNA KUFUFUKA KWA WAFU BASI KRISTO LAZIMA AWE BADO AMEKUFA."
"NA KAMA KRISTO BADO AMEKUFA BASI KUHUBIRI KWETU HAKUNA MAANA NA IMANI YENU NDANI YA MUNGU HAINA MAANA - N SISI MITUME NI WAONGO KWA SABABU TUMESEMA KUWA MUNGU ALIMFUFUA KRISTO KUTOKA KABURINI."
"KAMA KUWA MKRISTO KUNA THAMANI KWETU SISI SASA TU KWA MAISHA HAYA, TU VIUMBE WA KUSIKITISHA KABISA."
"LAKINI UKWELI NI KUWA KRISTO ALIFUFUKA KUTOKA MAUTI KWA HAKIKA NA AMEKUWA MMOJA WA MAMILIONI YA WATAKAORUDI HAI TENA SIKU MOJA."
"NA KUHUSU KUKUSANYWA KWA WATU WA MUNGU - SIKU YA KWANZA YA WIKI KILA MMOJA ANAFAA AWEKE KANDO KIWANGO FLANI CHA PESA KULINGANA NA MAPATO YAKE."
"IMANI YA BWANA IWE NANYI"


KWENYE BARUA YAKE YA PILI KWA KANISA HUKO KORINTHO PAULO ALIFURAHIA KUSIKIA KUWA WENGI WAO WALIJIBU NA KUTUBU JUU YA UASI WAO.
TUNAYE MUNGU WA AJABU - ANAYETUFARIJI NA KUTUTIA NGUVU KATIKA MAJARIBU YETU.
AFANYA HIVI ILI WENGINE WANAPOTESEKA TUTAWEZA KUWAPA FARAJA ILE ILE MUNGU AMETUPA SISI.
MTU YULE NILIYEANDIKA KUMHUSU AMEADHIBIWA VYA KUTOSHA NA UMOJA WENU KATIKA KUTOKUBALIANA NAYE.
SASA NI WAKATI WA KUMSAMEHEA NA KUMFARIJI - KAMA SIVYO ATAKUFA MOYO NA HATAWEZA KUPONA.
"NI MUNGU MWENYEWE KWA REHEMA ZAKE ALIYETUPA KAZI HII YA AJABU YA KUWAAMBIA WENGINE HABARI YAKE NJEMA, KWA HIYO HATUKATI TAMAA."
"KAMA INJILI IMEFICHWA KWA MTU YEYOTE NI KWA SABABU SHETANI, AMBAYE NI MUNGU WA UOVU WA ULIMWENGU HUU, AMEMPOFUSHA ASIWEZE KUONA MWANGA MTUKUFU WA INJILI."
"LAKINI HAZINA HII YA THAMANI IMEWEKWA KATIKA CHOMBO CHA KUHARIBIKA CHA MIILI YETU DHAIFU ILI KILA MTU AONE KUWA NGUVU TUKUFU NI KUTOKA KWA MUNGU WETU WALA SIO ZETU."
“PANDE ZOTE TWADHIHIKIKA, BALI HATUSONGWI."



"KWANI TWAJUA KUWA WAKATI HEMA HILI LA MILI YETU LITASHUSHWA, TUTAKUWA NA MILI MIPYA MBINGUNI."
"KWANI LAZIMA TUSIMAME MBELE YA KRISTO KUHUKUMIWA KWA MEMA NA MABAYA TULIYOYAFANYA KWA MILI YETU YA ULIMWENGUNI."
"MUNGU AMETUPA FADHILA YA KUWASIHI WATU WAPATANISHWE NAYE."
“KWANI MUNGU ALIKUWA NDANI YA KRISTO, AKIUREJESHA ULIMWENGU KWAKE YEYE, SIO KUHESABU DHAMBI ZA WANADAMU DHIDI YAO TENA – HUU NI UJUMBE WETU WA AJABU.”
"TUNAJARIBU KUISHI KWA NJIA AMBAYO HAKUNA ATAKAYEKOSA KUMPATA BWANA - ILI MTU YEYOTE ASIPATE KOSA KWETU NA KUMLAUMU BWANA."
"KWA KILA JAMBO TUNAJARIBU KUONYESHA TU WAHUDUMU WA KWELI WA MUNGU."
"KWA SABURI TUNAVUMILIA KUTESEKA NA TAABU NA SHIDA ZA KILA AINA."
"TUMETANDIKWA, TUMEFUNGWA GEREZANI, TUMEPATANA NA UMATI WENYE HASIRA, TUMEFANYA KAZI HADI KUCHOKA MNO, TUMEKESHA NA KUTOLALA KWA KUANGALIA NA TUMEKOSA CHAKULA."


"INGAWA NILIKUWA NAJUTA KWA MDA KUWATUMIA BARUA ILE, NIKIFIKIRIA ILIVYOLETA UCHUNGU KWENU."
"BALI SASA NAFURAHIA NILIITUMA, KWANI UCHUNGU ULIWAREGESHA KWA MUNGU."
"KWANI MUNGU SAA ZENGINE ATUMIA HUZUNI MAISHANI MWETU KUTUSAIDIA KUONDOKA KWA DHAMBI NA KUFUATA UHAI WA MILELE."
"KANISA ZA MAKEDONIA ZIMEKUWA ZIKIPITIA WAKATI MGUMU, LAKINI FURAHA YAO IKICHANGANYIKANA NA UMASIKINI WAO UMESABABISHA KUMIMINIKA KWA KUTOA KWA WENGINE."
"HAWAKUTOA TU WALICHOKUWA NACHO ILA KINGI ZAIDI - WAKIOMBA KUSHIRIKI KATIKA FURAHA YA KUWASAIDIA WAKRISTO KULE YERUSALEMU."
"WALIYAZIDI MATUMAINI YETU YA JUU KABISA, WAKIJITOLEA KWA BWANA MWANZO."
"MNA IMANI NYINGI MNO, WAHUBIRI WAZURI, KUSOMA, SHAUKU NA UPENDO KWETU - SASA NAWAHIMIZA KWA KUTOA NA FURAHA."
"MWAJUA UPENDO NA UKARIMU WA BWANA WETU YESU - INGAWA ALIKUWA TAJIRI SANA, ILA KUWASAIDIA AKAWA MASIKINI, ILI AWEZE KUWAFANYA MATAJIRI."



"NILIJIVUNA KWA WAMAKEDONIA KUWA MLIKUWA TAYARI KUTUMA SADAKA MWAKA MZIMA ULIOPITA."
"NI SHAUKU YENU ILIYOWACHOCHA KUSAIDIA KWA HIYO NATUMA WATU MBELE KUHAKIKISHA MKUSANYIKO WENU U TAYARI."
LAKINI KUMBUKA HAYA - MKITOA KIDOGO, MTAPATA KIDOGO. KILA MTU AJIAMULIE."
"MSILAZIMISHE MTU YEYOTE ATOE ZAIDI YA ATAKAVYO, KWANI WANAOTOA KWA FURAHA NDIO WANAOTUZWA NA MUNGU."
"MUNGU ATAWAPATIA VINGI ILI MUWEZE KUPEANA VINGI."
"KWA HIYO, VITU VIWILI VIZURI HUFANYIKA KAMA TUKIO LA KUTOA KWENU-WALIO NA HAJA WANASAIDIWA, NA WANAFURIKA NA SHUKRANI KWA MUNGU."
"NI KWELI KUWA MIMI NI MWANADAMU DHAIFU WA KAWAIDA LAKINI SITUMII MIPANGO NA MBINU ZA BINAADAMU KUSHINDA VITA VYANGU."
"NATUMIA SILAHA KUU ZA MUNGU KUANGUSHA NGOME ZA SHETANI NA KILA UKUTA UNAOWEZA KUJENGWA KUWAFANYA BINAADAMU WASIMPATE."



"SAMAHANI - NAOGOPA WALIMU HAWA WA UONGO WANAWEZA KUWAONGOZA KUTOKA KWA KUJITOLEA KWENU KWA BWANA WETU AMBAKO NI SAFI NA RAHISI, KAMA VILE HAWA ALIDANGANYWA NA SHETANI KWENYE SHAMBA LA EDEN."
"WANAHUBIRI YESU MWENGINE TOFAUTI NA TUNAYEHUBIRI."
"WANAJIVUNA KUWA WAO NI WAHEBRANIA - MIMI PIA NI MHEBRANIA."
"WANASEMA WAO NI WAISRAELI, WATU WALIOCHAGULIWA NA MUNGU - MI PIA NI MUISRAELI."
"WANASEMA WANAMTUMIKIA KRISTO - LAKINI NIMEMTUMIKIA ZAIDI!"
"NIMEFANYA KAZI KWA BIDII ZAIDI, KATIWA GEREZANI MARA NYINGI ZAIDI, NIMETANDIKWA NYAKATI NYINGI HAZIESABIKI NA KUKUMBANA NA KIFO MARA KWA MARA."
"MARA TANO WAYAHUDI WALINIPA MIJELEDI THELATHINI NA TISA."
"MARA TATU NILICHAPWA NA FIMBO. MARA MOJA NILIPIGWA MAWE."
"MARA TATU NILIHARIBIKIWA NA MELI. WAKATI MMOJA NILIKUWA KWENYE BAHARI JEUPE USIKU KUCHA NA SIKU NZIMA ILIYOFUATIA."
"MARA NYINGI NIMEKUWA HATARINI KWA MITO YA KUFURIKA NA WEZI NA WATU WANGU, WAYAHUDI, VILE VILE KUTOKA KWA MIKONO YA WAYUNANI."
"NIMEKUWA NA NJAA NA KIU - NIKATETEMEKA KWA BARIDI."
"LAKINI KAMA NI LAZIMA NIJIVUNE, AFADHALI NIJIVUNIE KUHUSU VITU VINAVYOONYESHA NILIVYO MNYONGE."


"MIAKA KUMI NA MINNE ILIYOPITA NILIPELEKWA JUU MBINGUNI - KAMA KWA MWILI AU ROHO, SIJUI."
"HUKO PARADISO NILISIKIA VITU VYA AJABU MNO HATA VINAPITA UWEZO WA MWANADAMU KUELEZA AU KUWEKA KATIKA MANENO."


"KISA HICHO NI KITU KINASTAHILI KUJIVUNIA JUU YACHO, ILA SITAFANYA HIVYO."
"KUNIFANYA NISIFURE KICHWA NA MAJIVUNO MUNGU ALINIPA MWIBA KWENYE MWILI WANGU, MJUMBE KUTOKA KWA SHETANI WA KUNIUMIZA NA KUNISUMBUA."
"MARA TATU TOFAUTI NILIMSIHI MUNGU KUUONDOA LAKINI KILA WAKATI ALISEMA, 'LA,. ILA NIKO NAWE; HILO NDIO UNALOHITAJI. NGUVU ZANGU ZINAONEKANA VIZURI KWA WATU WANYONGE.'"


"NINAOGOPA KUWA NITAKAPOKUJA MUNGU ATANINYENYEKEZA MBELE YENU NA NITAHUZUNIKA KWA KUWA WENGI WENU MUMETENDS DHAMBI MBELENI NA HAMJALI KUHUSU MAOVU MLIYOYATENDA."


"JIANGALIENI. JE MU WA KRISTO KWELI? MNAPITA MTIHANI?"
"MWASIKIA UWEPO WA KRISTO NA UWEZO WAKE ZAIDI NA ZAIDI NDANI YENU?"
"AMA MWAJIDAI TU KUWA WAKRISTO NA SIVYO KABISA?"
"NEEMA YA BWANA YESU KRISTO IWE NANYI WOTE."


PAULO ALIANZISHA KANISA KADHAA KUSINI MWA ROMA KATIKA MKOA WA GALATIA, AMBAYO NI UTURUKI SASA."
GALATIA
Konya
Iconium
Lystra
Derbe
Karaman
TURKEY
Adana
Tarsus
Mersin
Alanya
Anamur
Antakya
Antioch
Aleppo
SYRIA
Latakia
Nicosia
CYPRUS
Hama
Homs
PAULO ALIIANDIKA BARUA HII KUWAPINGA WALIMU WAONGO WALIOFUNZA KUWA WATU WALIFAA KUTII AMRI ZA SHERIA YA MUSA ILI KUPATA WOKOVU.
BARUA HII NDIO YA KIPEKEE ILIYOANDIKWA NA MTUME ISIYOKUWA NA PONGEZI KWA KWASOMAJI WAKE.
KUTOKA KITABU CHA WAGALATIA TUNAJIFUNZA KUWA MTUME PAULO ALIISHI UARABUNI MIAKA MITATU BAADA YA KUBADILI KWAKE.
BAADAYE ALIKUJA YERUSALEMU KUKUTANA NA KUJUANA NA MTUME PETERO.
PAULO ALISISITIZA KUWA KUHESABIWA-HAKI KWA IMANI NDANI YA YESU PEKE YAKE NDIYO HABARI NJEMA
LAKINI KAMA SISI AU MALAIKA KUTOKA MBINGUNI ATAHUBIRI INJILI MBALI NA ILE TULIWAHUBIRIA, WACHA WALAANIWE NA MUNGU!


"PETERO NA WENGINE WALIFAHAMU KUWA NILIKABIDHIWA KAZI YA KUHUBIRI INJILI KWA WAYUNANI - KAMA TU PETERO ALIVYOFANYA KWA WAYAHUDI."
"LAKINI PETERO ALIPOKUJA ANTIOKIA NILIMPINGA KWA UWAZI KWA SABABU ALIKATAA KULA NA WAYUNANI WAYAHUDI WALIPOKUJA."
"NILIMUAMBIA..."
WEWE NI MYAHUDI KWA KUZALIWA NA HUFATII TENA SHERIA ZA KIYAHUDI - MBONA WAJARIBU KUWAFANYA WAYUNANI WAZITII?
SISI WAKRISTO WAYAHUDI TWAJUA HATUWEZI KUWA SAWA NA MUNGU KWA KUTII SHERIA ZETU ZA KIYAHUDI - IMANI NDANI YA YESU KRISTO PEKE YAKE NDIYO INAYOWEZA KUONDOA DHAMBI.
KWANI KUPITIA SHERIA NILIKUFA KWA SHERIA NDIO NIMUISHIE MUNGU.
NIMESULUBIWA PAMOJA NA KRISTO WALA SIISHI TENA, BALI KRISTO AISHI NDANI YANGU.
UHAI NILIO NAO SASA KWENYE MWILI, NAISHI KWA IMANI NDANI YA MWANA WA MUNGU, ALIYENIPENDA AKAJITOA NAFSI YAKE KWA AJILI YANGU.


ENYI WAGALATIA WAPUMBAVU! NI NANI ALIYEWAROGA? MBELE YA MACHO YENU YESU KRISTO ALIONEKANA AMESULUBIWA.
MLIMPOKEA ROHO KWA KAZI ZA SHERIA AU KWA KUAMINI MLICHOKISIKIA?
BAADA YA KUANZA KWA NJIA YA ROHO, JE SASA MNAJARIBU KUMALIZA KWA NJIA YA KIMWILI?
"MAANDIKO YALITAZAMIA WAKATI HUU AMBAPO MUNGU ATAWAOKOA WAYUNANI KUPITIA IMANI."
"MUNGU ALIMUAMBIA IBRAHIM..."
NITAWABARIKI WALE KWA KILA MATAIFA WANAONI-AMINI KAMA UFANYAVYO.
"BASI NI NDIVYO ... WOTE WAMUAMINIO KRISTO WANASHIRIKI BARAKA ILE ALIYOIPOKEA IBRAHIM."
"HAKUNA AWEZAYE KUPATA FADHILA YA MUNGU KWA KUJARIBU KUZIWEKA SHERIA ZA KIYAHUDI KWA SABABU MUNGU ASEMA NJIA PEKEE YA KUWA SAWA MACHONI MWAKE NI KWA IMANI."
"HAKUNA MYAHUDI AU MYUNANI, MTUMWA AU ALIYE HURU, MUME WALA MKE, KWANI NYOTE MU WAMOJA KATIKA KRISTO."


"BABA AKIFA NA KUMUACHIA MWANAWE MALI NYINGI MWANA HUYO HAMSHINDI MTUMWA - KWA SABABU WANAOMSIMAMIA WATAMUAMBIA ATAKACHOFANYA HADI AWE MTU MZIMA."
"HIVYO NDIVYO ILIVYOKUWA NASI KABLA KRISTO AJE - TULIKUWA WATUMWA KWA SHERIA ZA KIYAHUDI."
"LAKINI KWA WAKATI ULIOFAA MUNGU ALIMTUMA MWANA WAKE, ALIYEZALIWA NA MWANAMKE, KAZALIWA KAMA MYAHUDI, KUTUNUNULIA UHURU TULIOKUWA WATUMWA KWA SHARIA ILI ATUTWAE KAMA WANA WAKE HALISI."
"KABLA NYINYI WAYUNANI HAMJAMJUA MUNGU, MLIKUWA WATUMWA WA MIUNGU AMBAYO HATA HAIPO."
"NA INAWEZEKANAJE KUWA MWATAKA KURUDI TENA KUWA WATUMWA WA DINI ISIYO NA MAANA YA KUJARIBU KUINGIA MBINGUNI KWA KUTII SHERIA ZA MUNGU?"
"MWAJARIBU KUPATA FADHILA KWA MUNGU KWA MKIFANYACHO AU MNACHOKOSA KUKIFANYA KWA SIKU FULANI AU MIEZI AU MISIMU AU MIAKA."
"NAWAOGOPEA. NAOGOPA KAZI YANGU YOTE KWENU NYINYI HAIKUWA NA THAMANI YOYOTE."


"KRISTO AMETUFANYA HURU - MSIWE WATUMWA KWA SHERIA NA SHEREHE ZA KIYAHUDI."
"KAMA MNATEGEMEA TOHARA NA KUZINGATIA SHERIA ZA KIYAHUDI KUWAWEKA SAWA NA MUNGU, BASI KRISTO HAWEZI KUWAOKOA."
"KWA USAIDIZI WA ROHO MTAKATIFU TUNATEGEMEA KIFO CHA KRISTO KIONDOE DHAMBI ZETU NA KUTUFANYA SAWA NA MUNGU."
"HATUNA HAJA KUWA NA WASI WASI JUU YA TOHARA AU KUTOTII SHEREHE ZA KIYAHUDI - TUNACHOHITAJI NI IMANI INAYOFANYA KAZI KUPITIA UPENDO PEKE YAKE."
MLIKUWA MNAENDELEA VIZURI SANA. NI NANI ALIYEINGILIA KUWAONDOA KUTOKA KUUFUATA UKWELI?
KAMA KWELI SIO MUNGU, KWANI AMEWAITA KWA UHURU NDANI YA KRISTO.
"MUMEPEWA UHURU MSIFANYE MAKOSA - BALI UHURU KUPENDANA NA KUTUMIKIANA."
"SHERIA YOTE YAWEZA KUJUMLISHWA KWA AMRI HII MOJA; WAPENDE WENZAKO UNAVYOJIPENDA MWENYEWE. TAHADHARI MSIHARIBIANE."
WAGALATIA 5


"MKRISTO AKISHINDWA NA DHAMBI NYINYI AMBAO NI WACHA MUNGU MSAIDIENI KURUDI KWENYE NJIA SAWA KWA UPOLE - MKIKUMBUKA INGALIKUWA NYINYI."
"SHIRIKINI KWENYE SHIDA NA TAABU ZENU."
"KUMBUKENI HAMUWEZI KUMPUUZA MUNGU MKAFAULU - SIKU ZOTE MTU ATAVUNA AINA YA MMEA ALIOUPANDA!"
"AKIPANDA KWA MWILI WAKE, APANDA MBEGU ZA UOVU NA ATAVUNA VUNO LA KIFO - LAKINI AKIPANDA MEMA YA ROHO ATAVUNA UHAI WA MILELE."
"NAANDIKA MANENO HAYA YA KUFUNGA NA MAANDISHI YANGU - ONA MAANDISHI YALIVYO MAKUBWA!"
WALE WANAOFUNZA TOHARA WANATAKA UMAARUFU NA KUEPUKA MATESO YANAYOKUJA KUTOKANA NA MSALABA WA KRISTO."
"HASHA, NISIONE FAHARI KWA KITU CHOCHOTE ILA MSALABA WA BWANA WETU YESU KRISTO."
"KWA AJILI YA MSALABA HUO, HAMU YANGU KWA KILA KINACHOVUTIA DUNIANI ILIMALIZWA ZAMANI."
"HAIJALISHI IKIWA TUMETAHIRIWA AU LA - MUHIMU NI KAMA KWELI TUMEBADILIKA KUWA MTU MPYA."



WAEFESO
BARUA KWA KANISA LA EFESO ILIANDIKWA WAKATI PAULO ALIPOKUWA GEREZANI ROMA, WAKATI FLANI KATI YA 60-62 B.K.
EFESO ILIKUWA MJII MKUU WA MKOA WA ROMA WA ASIA (UTURUKI YA SASA).
KUNA UWEZEKANO PRISILA NA AKILA WALIANZISHA KANISA HILI NA PAULO AKAWA MHUBIRI KWA MIAKA MITATU.
BARUA ILIKUWA YA KUWAKUMBUSHA WAUMINI JUU YA BARAKA BILA KIPIMO WALIZO NAZO KATIKA YESU - NA JINSI YA KUISHI KWA MWITIKO WA BARAKA HIZO.
"KWA WATAKATIFU WALIO EFESO, TUNAMSIFU MUNGU, BABA WA BWANA WETU YESU KRSITO ALIYETUBARIKI NA KILA BARAKA MBINGUNI KWA KUWA TU WA KRISTO."
BARUA HII PIA INAELEZEA SIRI KUU - AMBAYO WAUMINI WASO WAYAHUDI PIA WANGEKUWA WARITHI WA BARAKA NDANI YA KRISTO.
BARUA KUTOKA PAULO...
"TANGU NISIKIE KUHUSU IMANI YENU, SIJAACHA KUSHUKURU KWA SABABU YENU."
WAEFESO 1:1-16


"HAPO MWANZO MLIKUWA CHINI YA LAANA YA MUNGU KWA DHAMBI ZENU HUKU MKIMFUATA SHETANI."
"SOTE TULIKUWA HIVYO, TUKIFANYA KILA KITU KIOVU AMBACHO TAMAA YETU YA UOVU ILITUONGOZA KWACHO."
"LAKINI MUNGU ALIYE NA WINGI WA REHEMA ALITUPENDA HATA TULIPOKUWA WAFU KATIKA DHAMBI ZETU."
"ALITURUDISHIA MAISHA YETU ALIPOMFUFUA KRISTO KUTOKA KWENYE MAUTI-KWANI NI KWA NEEMA TUMEOKOLEWA."
"MLIKUWA WA MATAIFA NA KUITWA 'WACHAFU' NA WAYAHUDI."
"LAKINI SASA MU WA KRISTO ALIYEWAFANYA WAYAHUDI NA WAYUNANI JAMII MOJA,"
"MNASIMAMA KWENYE MSINGI WA MITUME NA MANABII PAMOJA NA YESU KRISTO KAMA JIWE KUU LA PEMBENI."
“TUNAUNGANISHWA PAMOJA NA KRISTO KUWA HEKALU MARIDADI LA MUNGU LINALOKUWA."


"MIMI PAULO, MTUMISHI WA KRISTO, NIKO HAPA GEREZANI KWA KUHUBIRI KUWA NYINYI WAYUNANI NI SEHEMU YA NYUMBA YA MUNGU."
"NA HII NI SIRI YA MUNGU - KUWA WAYUNANI WATAKUWA NA KIPANDE KIZIMA NA WAYAHUDI KATIKA UTAJIRI WOTE WATAKAORITHI WANA WA MUNGU; WOTE WANAALIKWA KWENYE KANISA LAKE.
"SABABU YAKE ILIKUWA KUONYESHA WAMILIKI WA MBINGUNI HEKIMA YA MPANGO WAKE - WA WAYAHUDI NA WAYUNANI WOTE KUUNGANISHWA PAMOJA KATIKA KANISA LAKE."
"NIKIWAZA HEKIMA YA MPANGO WAKE NASUJUDU NA KUMUOMBA BABA KUWA KUTOKANA NA UTAJIRI WAKE MTUKUFU ATAWAPA NGUVU KUU ZA ROHO WAKE MTAKATIFU."
"UTUKUFU UWE KWA MUNGU AWEZAYE KUFANYA ZAIDI YA TUNAVYOWEZA KUOMBA AU HATA KUOTA."
"APEWE UTUKUFU MILELE NA MILELE KWA NYAKATI ZISIZOPITA KWA SABABU YA MPANGO WAKE MKUU WA UKOMBOZI KUPITIA YESU KRISTO."


"NAWASIHI WAKATI NIMO HUMU GEREZANI KWA KUMTUMIKIA BWANA - MUISHI NA KUTENDA KWA NJIA INAYOSTAHILI WALE WALIOCHAGULIWA KWA BARAKA KAMA HIZI."
"KUWENI WANYENYEKEVU, NA WAPOLE, MUWE NA SABURI KATI YENU."
"SOTE TU SEHEMU ZA MWILI MMOJA, NA TUMEITWA KWA WAKATI MMOJA WA UTUKUFU UNAOKUJA."
"LAKINI KWA KILA MMOJA WETU NEEMA IMEPEANWA KAMA TU VILE AMBAVYO KRISTO ALIVYOAMUA KUIPEANA."
"ALIWAPA WENGINE KUWA MITUME, WENGINE KUHUBIRI VYEMA, WENGINE WAINJILISTI, NA WENGINE WACHUNGAJI NA WALIMU KUWATAYARISHA WATU WA MUNGU KWA HUDUMA."
"ACHENI KUDANGANYANA. KAMA YEYOTE ANAIBA LAZIMA AWACHE NA KUTUMIA MIKONO YAKE KUFANYA KAZI YA HAKI NA KUWASAIDIA WENYE MAHITAJI."
"MSIACHE JUA LITUE KAMA BADO MNA HASIRA-MALIZANA NAYO HARAKA ILI MSIMPE IBILISI KIPENYO."
"ACHENI KUWA WADHALIFU, WENYE HAMAKI NA HASIRA."
"BADALA YAKE MUWE WAKARIMU, MSAMEHEANE, KAMA MUNGU ALIVYOWASAMEHEA KWA KUWA MU WA KRISTO."
WAEFESO 4


"KUSIWE NA DHAMBI YA NGONO KATI YENU, UCHAFU, UCHOYO WALA MAZUNGUMZO MACHAFU KATI YENU - BADALA YAKE MSHUKURU."
"MSITENDE BILA MAWAZO ILA JARIBU KUJUA NA KUFANYA KILE BWANA ATAKA MFANYE."
"MSINYWE MVINYO MWINGI SANA, BADALA YAKE MJAZWE NA ROHO MTAKATIFU."
"ZUNGUMZISHANENI KUMHUSU BWANA NA MUPIGE MUZIKI MIOYONI KWA BWANA - MUWE NA SHUKRANI WAKATI WOTE KWA KILA KITU KWA MUNGU NA BABA YETU KATIKA JINA LA BWANA WETU YESU KRISTO."
"MHESHIMU KRISTO KWA KUNYENYEKEANA."
"ENYI WAKE LAZIMA MHESHIMU UONGOZI WA WAUME WENU VILE AMBAVYO MNANYENYEKEA KWA BWANA."
"NANYI WAUME, WAPENDENI WAKE ZENU VILE AMBAVYO KRISTO ALIMPENDA KANISA ALIPOKUFA KWA AJILI YAKE."
"MUME LAZIMA AMPENDE MKEWE ANAVYOJIPENDA MWENYEWE; NA MKE LAZIMA AHAKIKISHE ANAMTII NA KUMHESHIMU MUMEWE."


"WATOTO WATII WAZAZI WENU MAANA HII NDIYO HAKI."
"NANYI WAZAZI - MSIENDELEE KUWAKEMEA NA KUWACHOKOZA WATOTO WENU - BALI, WALEENI KATIKA ADABU YA UPENDO."
"ENYI WATUMWA, WATIINI MABWANA ZENU; KUWA NA HAMU YA KUWAPA UTUMISHI BORA."
"NANYI MABWANA LAZIMA MUWATENDEE WATUMWA WENU MEMA."
"HATIMAYE, VAENI SILAHA ZOTE ZA MUNGU MPATE KUWEZA KUZIPINGA HILA ZOTE ZA SHETANI."
"TUMIA MSHIPI WA UKWELI NA DIRII YA HAKI YA MUNGU."
"VAENI VIATU VYA KUWAHARAKISHA MKIHUBIRI HABARI NJEMA YA AMANI."
"KWA KILA VITA MTAHITAJI IMANI KAMA NGAO KUSIMAMISHA MISHALE YA MOTO MLIYOLENGWA NA SHETANI."
"NA MTAHITAJI CHAPEO YA WOKOVU NA UPANGA WA ROHO - AMBAO NI NENO LA MUNGU."
"OMBENI WAKATI WOTE NA MUULIZE MUNGU CHOCHOTE KINACHOAMBATANA NA MATAKWA YA ROHO MTAKATIFU."
"...NA MUOMBE NIENDELEE KUONGEA KWA UJASIRI KWA NIAMBA YAKE HATA HAPA GEREZANI."

"THE BIBLE EXPLAINED IN EVERY LANGUAGE."








**SUPERBIBLE.TV**